**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

# TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA WALIOFANYA MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2023

107 DINI

Kimetayarishwa na

Baraza la Mitihani la Zanzibar

S. L. P. 3070,

Zanzibar.

©Baraza la Mitihani la Zanzibar, 2024

Haki zote zimehifadhiwa

# YALIYOMO

DIBAJI ..... iv
1.0 UTANGULIZI ..... 1
2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA ..... 1
3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI ..... 1
3.1 SEHEMU A: QUR-AN NA TAFSIRI ..... 1
3.1.1 Swali la 1: Qur-an na Tafsiri ..... 1
3.1.2 Swali la 2. Tafsiri ya Qur-an ..... 4
3.2 SEHEMU B: TAWHIDI ..... 8
3.2.1 Swali la 3: Kulinganisha ..... 8
3.2.2 Swali la 4: Kuandika “K” au “S” ..... 9
3.3 SEHEMU C: HADITHI ..... 11
3.3.1 Swali la 5: Hadithi (Haki za njia) ..... 11
3.3.2 Swali la 6: hadithi ..... 13
3.4 SEHEMU D: FIQHI NA MAADILI ..... 15
3.4.1 Swali la 7: Kujaza mapengo (Maadili) ..... 15
3.4.2 Swali la 8: Kujaza mapengo (Fiqhi) ..... 17
3.4.3 Swali la 9: Fiqhi ..... 19
3.4.4 Swali la 10: Tohara ..... 22
3.5 SEHEMU E: TAREKHE ..... 24
3.5.1 Swali la 11: Tarekhe ..... 24
3.5.2 Swali la 12: Kuhama Makka Mtume (S.A.W) kuelekea Madina ..... 28
4.0 HITIMISHO ..... 31
5.0 MAPENDEKEZO ..... 31
VIAMBATANISHO ..... 32

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Zanzibar limeandaa taarifa ya tathmini ya ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kuingilia Kidato cha Kwanza katika somo la Dini ya Kiislamu mwaka 2023. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu kwa wanafunzi, walimu, wazazi, waandaaji wa sera, watunga mitaala na jamii kwa ujumla kuhusu ufaulu wa watahiniwa kwa somo hilo.

Mtihani wa kuingilia Kidatu cha Kwanza ni kigezo cha miaka mitatu ya Elimu ya Msingi ambapo wanafunzi hukusudiwa kupimwa ili kuona ni kwa namna gani wameweza kukumbuka masomo yao ya Darasa la tano (5) hadi la saba (7). Hivyo, mtihani huu ni maandalizi tosha kwa ajili ya Elimu ya Sekondari.

Pamoja na hayo uchambuzi huu umeonesha mambo mbali mbali ambapo yaliwafanya watahiniwa kushindwa kufikia lengo la maswali hayo. Pia umeonesha changamoto ambazo zimewafanya watahiniwa kushindwa kufahamu matakwa ya swali kutokana na maarifa madogo au ujuzi waliokuwa nao ni mdogo katika fani za Qur-an, Tafsiri, Tawhidi, Hadithi, Maadili, Fiqhi na Tareikh.

Aidha, uchambuzi umeonesha vielelezo vya watahiniwa jinsi walivyojibu vizuri au vibaya. Mwisho, uchambuzi huu umetumia Jadweli ambazo zimebainishwa kwa rangi tofauti. Jadweli hizo zinaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa kila swali.

Hivyo, ni imani ya Baraza kuwa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii yatachukuliwa na wadau wa Elimu na kuyafanyia kazi kwa lengo la kuinua ufaulu wa somo la Dini katika mitihani yote inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Zanzibar linatoa shukurani kwa Maafisa Mitihani na wote walioshiriki katika kukamilisha taarifa hii.

**Dkt. RASHID .A. MUKKI**

**MKURUGENZI**
**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**
**ZANZIBAR**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa ya uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa kuingia Kidato cha Kwanza kwa somo la Dini mwaka 2023. Mtihani ulitungwa kwa kuzingatia muhtasari wa Zanzibar wa mwaka 2009 na 2022 na kufuata muundo wa mtihani wa Darasa la Saba wa Baraza la Mitihani la Zanzibar wa mwaka 2022.

Mtihani huu ulikuwa na maswali kumi na mbili (12) yaliyogawanywa katika sehemu A, B, C, D na E. Sehemu A, B na C ilikuwa ni ya lazima ambapo watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu D ilikuwa na maswali manne (4) ambapo watahiniwa walitakiwa wachague maswali matatu (3) na sehemu E ilikuwa na maswali mawili (2) na watahiniwa walitakiwa kujibu swali moja (1) tu.

## 2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA

Idadi ya watahiniwa waliofanyiwa Tathmini ni **4,710** sawa na asilimia **10.84** ya watahiniwa **43,458** waliosajiliwa kufanya mtihani wa somo hili. Uchambuzi kwa kila swali ulizingatia viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni vibaya, wastani na vizuri, ambapo vibaya ni kuanza alama 0 hadi 20, wastani 21 hadi 60 na vizuri 61 hadi 100. Ufaulu huo umeoneshwa kupitia jadweli kwa kutumia rangi tatu ambazo ni: Kijani ambayo inawakilisha vizuri, manjano inawakilisha wastani na nyekundu inawakilisha vibaya.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

Sehemu hii, inaonesha maswali yaliyojibiwa na watahiniwa katika sehemu A, B, C, D na E. Pia inawakilisha asilimia ya watahiniwa waliojibu maswali pamoja na asilimia ya waliopata vibaya, wastani na vizuri. Mwisho, vielelezo vya watahiniwa waliojibu vizuri na vibaya vimeambatanishwa

### 3.1 SEHEMU A: QUR-AN NA TAFSIRI

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali mawili (2) yaliyotokana na mada ya Qur-ani na tafsiri, ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Swali la kwanza (1) lilikuwa na alama (10) na swali la pili (2) lilikuwa na alama (10). Hivyo katika sehemu hii kulikuwa na jumla ya alama (20).

#### 3.1.1 Swali la 1: Qur-an na Tafsiri

Swali la kwanza lilitokana na mada ya Qurani na tafsiri ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu swali hilo. Swali hili lilikuwa na vipengele kumi (10) kuanzia (i) hadi (x).

Kipengele (i) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutaja sura aliyoteremshiwa Mtume (S.A.W) yote nzima miongoni mwa sura alizopewa kuchagua ambazo ni:-

A. Suratul Adiyat B. Suratul Alaq

C. Suratul Fat - ha D. Suratul Tin

Kipengele (ii) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutoa maana ya neno “ صِّلَ ” miongoni
حُ
mwa maneno aliyopewa.

A. Yatakapochukuliwa B. Yatakapodhihirishwa

C. Yatakaposokotwa D. Yatakapotolewa

Kipengele (iii) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutaja sehemu iliyoteremshwa suratul bayyinah kulingana na majibu yafuatayo aliyopewa.

A. Madina B. Makka C. Misri D. Sham

Kipengele (iv) cha swali kilimtaka mtahiniwa aeleze aya za mwanzo alizoteremshiwa Mtume (S.A.W) zilimtaka afanye nini?

A. Apigane Jihadi B. Asome

C. Alishe D. Atangaze Dini

Kipengele cha (v) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutaja vigawanyo vya hukumu ya nuni sakina na tanwini kulingana na majibu aliyopewa kama ifuatavyo:-

A. Mawili B. Matatu C. Manne D. Matano

Kipengele cha (vi) cha swali kilimtaka mtahiniwa kuainisha hukumu ya nuni sakina na tanwini katika aya aliyopewa kwa kuchagua jawabu sahihi katika hukumu alizopewa.

A. Id-Gham B. Idh-Har C. Ikhfau D. Iqlab

Kipengele cha (vii) cha swali kilimtaka mtahiniwa aeleze maana ya Iqlaab kilugha kwa kuchagua jawabu kutokana na maneno aliyopewa ambayo ni:-

A. Kubainisha B. Kudhihirisha C. Kuficha D. Kugeuza

Kipengele cha (viii) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutaja idadi ya herufi za Id-gham katika idadi alizopewa.

A. 4 B. 6 C. 10 D. 15

Kipengele cha (ix) cha swali kilimtaka mtahiniwa ainishe jina la maneno ya kitabu cha Mwenyezi Mungu yaliyokuwa hayajaharibiwa kutokana na vitabu alivyopewa kuchagua.

A. Injil B. Qur-an C. Taurati D. Zabouri

Kipengele cha (x) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutaja sehemu iliyoteremshwa suratu lail pamoja na kutaja idadi ya aya za sura hiyo kwa kuchagua katika majawabu yafuatayo:-

A. 21- Madina B. 21 – Makka C. 21 – Sham D, 21 - Syria

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kujibu maswali yanayotokana na Qur-ani na tafsiri yake.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,700** sawa na asilimia **99.79** na **10** sawa na asilimia **0.21** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 1a.


**Jadweli nambari 1a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 435 | 9.26 | 3,334 | 70.93 | 931 | 19.81 | 4,265 | 90.74 |

Takwimu za Jadweli nambari 1a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **70.93** upo katika kiwango cha wastani ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri kwa asilimia **90.74.**

Aidha, watahiniwa **435** sawa na asilimia **9.26** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana hawakuwa na maarifa mazuri juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 1.1.

## Kielelezo 1.1 (Kibaya)



JAWABU

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | D | B | D | B | D | C | A | B | A |

Kielelezo nambari 1.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya, kwa kukosa katika vipengele vyote vya majibu yake isipokuwa kipengele cha (ix). Hii ni kwa sababu mtahiniwa hakuweza kuchaguwa jibu lililo sahihi.
Aidha, watahiniwa **931** sawa na asilimia **19.81** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 1.2

**Kielelezo 1.2 (kielelezo kizuri)**

JAWABU

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| C | B | A | B | C | C | D | B | B | B |

Kielelezo nambari 1.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na ufahamu na ufahamu mzuri juu ya alichoulizwa kiasi ambacho ameweza kuandika majibu yote kwa usahihi.

### 3.1.2 Swali la 2. Tafsiri ya Qur-an

Swali hili lilikuwa na vipengele viwili (2) (a) na (b) na kila kipengele kilichukua alama tano (5). Kipengele (a) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutafsiri aya alizopewa. Kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kupanga tafsiri ya aya alizopewa.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ujuzi na maarifa ya mtahiniwa katika kutafsiri Qur-ani.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,694** sawa na asilimia **99.66** watahiniwa **16** sawa na asilimia **0.34** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 1b.

**Jadweli Nambari 1b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,378 | 50.66 | 1,538 | 32.77 | 778 | 16.57 | 2,316 | 49.34 |

Takwimu za jadweli nambari 1b zinaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **16.57** upo katika kiwango cha vizuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **49.34**.

Aidha watahiniwa **2,378** sawa na asilimia **50.66** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 2.1.

**Kielelezo 2.1 (kielelezo kibaya)**

2. a) Lete tafsiri ya aya zifuatazo:-

١. يَوْمَئِذٍ تُحَدِّثُ أَخْبَارَهَا.

Siryo hiryo karibuni mtajua

٢. إِنَّ الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا وَعَمِلُوا الصَّٰلِحَٰتِ أُولَٰئِكَ هُمْ خَيْرُ الْبَرِيَّةِ.

Siryo hiryo! Lau kamamnajua elimuya yakini.

Activate Wind

٣. فَأُمُّهُ هَاوِيَةٌ.

kishasi~~hiryo~~ Siryo hiryo! karibuni hiri mtaju a

٤. فَوَسَطْنَ بِهِ جَمْعًا.

Kumekushughulisheni kutafuta wingi wa mali na watoto

٤. فَوَسَطْنَ بِهِ جَمْعًا.

Kumekushughulisheni kutafuta wingi wa mali na watoto

٥. ثُمَّ لَتُسْئَلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيْمِ.

mpaka yamekupitieni mauti (mmeingia makaburini)

b) Panga tafsiri ya aya zifuatazo kwa kuandika herufi zake ndani ya sanduku lililopo chini kwa kufuata mpangilio.

A. Sivyo hivyo! Lau kama mnajua elimu ya yakini.

B. Sivyo hivyo karibuni mtajua.

C. Kumekushughulisheni kutafuta wingi wa mali na watoto.

D. Kisha sivyo hivyo! Karibuni hivi mtajua.

E. Mpaka yamekufikieni mauti (mmeingia makaburini).

**JAWABU**

| i. | ii. | iii. | iv. | v. |
|---|---|---|---|---|
| B | A | D | C | E |

Kielelezo nambari 2.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu katika kipengele cha kwanza alitakiwa kutafsiri aya alizopewa, badala yake aliandika tafsiri ya aya alizopewa kuzipanga.

Aidha watahiniwa **778** sawa na asilimia **16.57** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na ujuzi juu ya kile walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 2.2

**Kielelezo (2.2) ( kizuri)**

2. a) Lete tafsiri ya aya zifuatazo:-

١. يَوْمَئِذٍ تُحَدِّثُ أَخْبَارَهَا.

Siku hiyo ardhi itahadithia habari zake

٢. إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّٰلِحَٰتِ أُولَٰئِكَ هُمْ خَيْرُ الْبَرِيَّةِ.

Ispokuwa wale waliomini na wakatenda mema hao ndio viumbe ~~waovu~~ wema.

٣. فَأُمُّهُ هَاوِيَةٌ.

Ataingia katika moto wa hawiya

٤. فَوَسَطْنَ بِهِ جَمْعًا.

Wakaingia kati ya kundi moja la maadui wakapigana.

٥. ثُمَّ لَتُسْأَلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيمِ.

Kisha mtaenda kuulizwa juu ya neema mlizo neemeshwa.

b) Panga tafsiri ya aya zifuatazo kwa kuandika herufi zake ndani ya sanduku lililopo chini kwa kufuata mpangilio.

A. Sivyo hivyo! Lau kama mnajua elimu ya yakini.

B. Sivyo hivyo karibuni mtajua.

C. Kumekushughulisheni kutafuta wingi wa mali na watoto.

D. Kisha sivyo hivyo! Karibuni hivi mtajua.

E. Mpaka yamekufikieni mauti (mmeingia makaburini).

**JAWABU**

| i. | ii. | iii. | iv. | v. |
|---|---|---|---|---|
| C | E | B | D | A |

Kielelezo nambari 2.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na ufahamu na ufahamu mzuri juu ya tafsiri ya qur-ani kiasi ambacho ameweza kuandika majibu yote kwa usahihi.

### 3.2 SEHEMU B: TAWHIDI

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali mawili (2) kutoka katika mada ya Tawhidi. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote mawili (2) na kila swali lilikuwa na alama kumi (10), hivyo katika sehemu hii inafanya jumla ya alama zote kuwa ni ishirini (20).

#### 3.2.1 Swali la 3: Kulinganisha

Swali hili lilikuwa la kulinganisha baina ya orodhsa "A" na orodha "B" kwa kuchagua jawabu kutoka orodha "B". Orodha "A" ilikuwa ni tafsiri ya majina ya Mwenyezi Mungu, ambako kulikuwa na vipengele kumi (10) (i) mpaka (x) na kila kipengele kilichukua alama moja (1). Orodha "B" ilikuwa na majina ya Mwenyezi Mungu yafuatayo

A. Al-Mutakabbiru B. Al-Muhayminu C.Al-jabbaru D. Al-Rahiymu

E. Al-Maliku F. Al-Rahmaanu G. As Salaam H. Al-Quddusu

I. Al-Muuminu J. Al-Aziyzu K. Al-Qaadiru L. Al-Ghaniyyu

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kutafsiri Qur-ani.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,695** sawa na asilimia **99.68** watahiniwa **15** sawa na asilimia **0.32** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 2a.

**Jadweli Nambari 2a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 2.5 | | 3 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,111 | 44.96 | 2,242 | 47.76 | 342 | 7.28 | 2,584 | 55.04 |

Jadweli nambari 2a linaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **7.28** upo katika kiwango cha vizuri, hata hivyo ufaulu wa jumla umekuwa wa wastani kwa asilimia **55.04.**

Aidha, watahiniwa **2,111** sawa na asilimia **44.96** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na kumbu kumbu pamoja na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 3.1.

**Kielelezo (3.1) (kibaya)**

**JAWABU**

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| i | iii | ii | v | iv | vi | v | vii | viii | ix |

Kielelezo nambari 3.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu inaonekana hakuwa na maarifa juu ya alichoulizwa. Mtahiniwa huyu alitakiwa kujibu swali hili kwa kuandika kwa herufi zilizoainishwa katika orodha "B", badala yake kajibu swali hili kwa kutumia nambari za kirumi.

Aidha, watahiniwa **342** sawa na **asilimia 7.28** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 3.2

**Kielelezo (3.2) ( kizuri)**

**JAWABU**

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| F | D | E | H | G | I | B | J | C | A |

Kielelezo nambari 3.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na ufahamu mzuri juu ya majina ya Mwenyezi Mungu ambapo ameweza kuandika majibu yote kwa usahihi.

### 3.2.2 Swali la 4: Kuandika "K" au "S"

Swali hili lilikuwa na vipengele kumi (10) na kila kipengele kilichukua alama moja (1). Swali hili katika vipengele vyake vyote vilimtaka mtahiniwa kuandika kweli kwa herufi (K) au sikweli kwa herufi (S). Swali hili lilitokana na mada ya Tawhidi.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika mada ya unafiki, majina ya Mwenyezi Mungu na nguzo za imani.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,697** sawa na asilimia **99.72** watahiniwa **13** sawa na asilimia **0.28** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 2b.


**Jadweli Nambari 2b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 122 | 2.60 | 1,073 | 22.84 | 3,502 | 74.56 | 4,576 | 97.40 |

Jadweli nambari 2b linaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **2.60** upo katika kiwango cha vibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa mzuri kwa asilimia **97.40.**

Aidha, watahiniwa **122** sawa na asilimia **2.60** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada iliyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 4.1.

**Kielelezo (4.1) (kibaya)**



JAWABU

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | C | B | D | F | R | E | G | A | C |

Kielelezo nambari 4.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu inaonekana hakuwa na ufahamu pamoja na maarifa juu ya alichoulizwa. Mtahiniwa huyu alitakiwa kujibu swali hili kwa kuandika (K) ikiwa ni kweli au (S) ikiwa sikweli, badala yake kajibu swali hili kwa kutumia herufi zake mwenyewe.

Aidha, watahiniwa **3,502** sawa na asilimia **74.56** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 4.2

**Kielelezo (4.2) ( kizuri)**


JAWABU

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | K | K | K | S | S | K | K | S | K |

Kielelezo nambari 4.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na ufahamu mzuri juu ya majina ya Mwenyezi Mungu, nguzo za imani na unafiki ambapo ameweza kuandika majibu yote kwa usahihi.

**3.3 SEHEMU C: HADITHI**

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (2) kutoka katika mada ya hadithi. Mtahiniwa alitakiwa ajibu maswali yote mawili ambayo kila swali lilikuwa na alama kumi (10 hivyo kufanya jumla ya alama katika sehemu hii kuwa ni alama ishirini (20).

**3.3.1 Swali la 5: Hadithi (Haki za njia)**

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kukamilisha hadithi kwa kujaza nafasi zilizoachwa waz kwa kuchagua jawabu sahihi kutoka katika maneno aliyopewa.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kuhifadhi na kuandika hadithi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,661** sawa na asilimia **97.96** watahiniwa **49** sawa na asilimia **2.04** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 3a.


**Jadweli Nambari 3a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 3,037 | 65.16 | 839 | 18.00 | 785 | 16.84 | 1,624 | 34.84 |

Jadweli nambari 3a linaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **16.84** upo katika kiwango cha vizuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **34.84.**

Aidha watahiniwa **3,037** sawa na asilimia **65.16** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 5.1.

**Kielelezo (5.1) (kibaya)**



5. Kamilisha hadithi ifuatayo kwa kuchagua jawabu lililo sahihi katika Sanduku.


نَهْيُ – غَضُّ – المُنْكَر – الأذى – أبَيْتُمْ – لَنَا – فَأعْطُوا – نَتَحَدَّثُ – الجُلُوْس – رَدُّ - فِيْنَا.

عَنْ أبِيْ سَعِيْدٍ الخُدْرِيِّ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ قَالَ: عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: إِيَّاكُمْ وَ ____ فِيْ الطُّرُقَاتِ، قَالُوْا يَارَسُوْلَ اللهِ! مَا ____ بُدٌّ مِنْ مَجَالِسِنَا ____ فِيْهَا، قَالَ: فَإِذَا ____ إِلاَّ المَجْلِسَ ____ الطَّرِيْقَ حَقَّهُ، قَالُوْا وَمَا حَقُّهُ؟ قَالَ: ____ البَصَرِ، وَكَفُّ ____ وَ ____ السَّلاَمِ، وَالأَمْرُ بِالمَعْرُوْفِ وَ ____ عَنِ ____. (رَوَاهُ مُسْلِمٌ)

Kielelezo nambari 5.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu inaonekana hakuwa na maarifa ya kutosha juu ya alichoulizwa. Mtahiniwa huyu alitakiwa kukamilisha hadithi kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi, mtahiniwa huyu alijaribu kujaza nafasi hizo kwa kuchagua maneno aliyopewa lakini alikosa zote isipokuwa nafasi ya mwisho aliweza kujaza kwa usahihi wake.

Aidha watahiniwa **785** sawa na asilimia **16.84** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 5.2

**Kielelezo (5.2) ( kizuri)**



5. Kamilisha hadithi ifuatayo kwa kuchagua jawabu lililo sahihi katika Sanduku.

نَهْيُ – غَضُّ – المُنْكَر – الأذى – أبَيْتُمْ – لَنَا – فَأعْطُوا – نَتَحَدَّثُ – الجُلُوْس – رَدُّ - فِيْنَا.

عَنْ أبِيْ سَعِيْدٍ الخُدْرِيِّ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ قَالَ: عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: إِيَّاكُمْ وَ ____ فِيْ الطُّرُقَاتِ، قَالُوْا يَارَسُوْلَ اللهِ! مَا ____ بُدٌّ مِنْ مَجَالِسِنَا ____ فِيْهَا، قَالَ: فَإِذَا ____ إِلاَّ المَجْلِسَ ____ الطَّرِيْقَ حَقَّهُ، قَالُوْا وَمَا حَقُّهُ؟ قَالَ: ____ البَصَرِ، وَكَفُّ ____

وَ ___ رَدِّ ___ السَّلَامِ، وَالأَمْرُ بِالمَعْرُوفِ وَ ___ نَهْيٍ ___ عَنِ
___ المُنْكَرِ ___. (رَوَاهُ مُسْلِمٌ)

Kielelezo nambari 5.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na maarifa mazuri juu ya hadithi inayozungumzia haki za njia, ambapo alieweza kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa usahihi wake.

### 3.3.2 Swali la 6: hadithi

Swali hili lilikuwa na vipengele viwili (2) (a) na (b) na kila kipengele kilichukua alama tano (5). Kipengele (a) cha swali kilimtaka mtahiniwa kuleta maana ya maneno aliyoopewa. Kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kutoa mafunzo yanayopatikana katika hadithi ya uchamungu.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kuleta maana na kutoa mafunzo ya hadithi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,510** sawa na asilimia **95.75** watahiniwa **200** sawa na asilimia **4.25** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 3b.

**Jadweli Nambari 3b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,830 | 40.58 | 1,852 | 41.06 | 828 | 18.36 | 2,680 | 59.42 |

Takwimu za jadweli nambari 3b zinaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **18.36** upo katika kiwango cha vizuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **59.42.**

Aidha, watahiniwa **1,830** sawa na asilimia **40.58** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 6.1.

**Kielelezo (6.1) (kibaya)**

6. a) Lete maana ya maneno yafuatayo:

| MAANA | NENO |
|---|---|
| Kisha si vyohivyo karibuni mtajua | اِتَّقِ اللهِ -1 |
| Siyo hivyo karibuni mtajua | السَّيِّئَةَ -2 |
| Mpaka yame kufikeni mauti | تَمْحُوْهَا -3 |
| Lau kama mnajua elimu ya yakini | خَالِقِ -4 |
| Mmeingia makaburini | خُلُقٍ -5 |

b) Toa mafunzo mawili (2) yanayotokana na hadithi ya ucha Mungu.

i. Kisha siyo hivyo karibuni mtajua

ii. Lau kama mnajua elimu ya yakini


Kielelezo nambari 6.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu inaonekana hakuwa na maarifa ya kutosha juu ya alichoulizwa. Mtahiniwa huyu alitakiwa kwa mfano katika kipengele (a) kuandika maana ya maneno yanayotokana na hadithi ya haki za njia, badala yake ameandika tafsiri ya Qur-ani aliyopewa kuipanga katika swali la (2b).

Aidha watahiniwa **828** sawa na asilimia **18.36** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa ya kutosha juu ya hadithi ya uchamungu kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 6.2.

**Kielelezo (6.2) ( kizuri)**

6. a) Lete maana ya maneno yafuatayo:

| MAANA | NENO |
|---|---|
| Mwogope Allah | اِتَّقِ اللهِ -1 |
| ~~Jema~~ Mabaya | السَّيِّئَةَ -2 |
| Yatafuata | تَمْحُوْهَا -3 |
| Kuishi | خَالِقِ -4 |
| Tabia | خُلُقٍ -5 |



b) Toa mafunzo mawili (2) yanayotokana na hadithi ya ucha Mungu.

i. Tunatakiwa tumche Allah (S.a.w)

ii. Tufute mabaya yaliyotangulia kwa kufanya mambo mema.

Kielelezo nambari 6.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na maarifa mazuri juu ya hadithi ya ucha mungu, ambapo katika kipengele (a) aliweza kuandika maana ya maneno aliyopewa kwa usahihi wake na kukosa katika nambari (3), kwa upande wa kipengele (b) ameweza kutoa mafunzo kwa vizuri.

### 3.4 SEHEMU D: FIQHI NA MAADILI

Katika sehemu hii kulikuwa na maswali manne (4) kutoka katika mada ya Fiqhi na Maadili. Watahiniwa walitakiwa kuchagua maswali matatu tu (3) katika sehemu hii ambayo swali la saba (7) lilikuwa la lazima. Kila swali katika sehemu hii lilikuwa na alama kumi (10) ambapo ilifanya jumla ya alama zote kuwa ni thelathini (30).

#### 3.4.1 Swali la 7: Kujaza mapengo (Maadili)

Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) (a) mpaka (e) na kila kipengele kilichukua alama mbili (2). Swali hili lilikuwa la maadili na alitakiwa mtahiniwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima matumizi na maarifa ya mtahiniwa katika maadili.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,662** sawa na asilimia **98.98** watahiniwa **48** sawa na asilimia **1.02** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 4a.

**Jadweli Nambari 4a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 570 | 12.23 | 2,808 | 60.23 | 1,284 | 27.54 | 4,092 | 87.77 |

Takwimu za jadweli nambari 4a zinaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **12.23** upo katika kiwango cha vibaya na kupelekea ufaulu wa jumla kuwa mzuri kwa asilimia **87.77.**

Aidha, watahiniwa **570** sawa na asilimia **12.23** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 7.1.

**Kielelezo (7.1) ( kibaya)**

7. Kamilisha mapengo kwa kuweka jawabu sahihi.

a) Kutoamrisha mema na kukataza Mtaa ______ kunachangia kuporomoka kwa Kuoporomoka.

b) Qur-ani na Kuta ni miongoni mwa msingi ya maadili moto

c) Muislamu anatakiwa anatakiwa na tabia mata


d) Uisilamu unakataza kukaa Kutua kwa jinsia mbili za watu

e) Mwanamke wa kiislamu hatakiwi kudhihirisha amata yake akiwa ma ya nyumba yake.

Kielelezo nambari 7.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana hakuwa na maarifa ya kutosha juu ya alichoulizwa. Mtahiniwa huyu alitakiwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika maneno yanayoendana na sentensi za maadili alizopewa, badala yake amejaza nafasi hizo kwa kuandika maneno yasiyoleta maana kulingana na sentensi alizopewa na kupelekea kufanya vibaya katika swali hili.

Aidha watahiniwa **1,284** sawa na asilimia **27.54** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya maadili kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 7.2.

**Kielelezo (7.2) ( kizuri)**


7. Kamilisha mapengo kwa kuweka jawabu sahihi.

a) Kutoamrisha mema na kukataza mabaya kunachangia kuporomoka kwa uislamu.

b) Qur-ani na hadithi ni miongoni mwa msingi ya maadili mema

c) Muislamu anatakiwa kuwa na tabia njema

d) Uisilamu unakataza kukaa faragha kwa jinsia mbili za watu wanaoweza kuoana

e) Mwanamke wa kiislamu hatakiwi kudhihirisha maumbile yake akiwa nje ya nyumba yake.

Kielelezo nambari 7.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na maarifa pamoja na ufahamu mzuri juu ya mada ya maadili, ambapo ameweza kujaza nafasi zote zilizoachwa wazi kwa usahihi wake.

### 3.4.2 Swali la 8: Kujaza mapengo (Fiqhi)

Swali hili lilikuwa na vipengele vinne (4) (a) mpaka (d), swali hili lilikuwa la zaka. Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kueleza maana ya zaka kisheria.

Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa ainishe ni watu wa aina ngapi wanaostahiki kupewa zaka kwa mujibu wa Qur-ani.

Kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa ataje makundi manne ya mwanzo ya watu wanaostahiki kupewa zaka.

Kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa ataje sifa ya mali inayotakiwa kutolewa zaka.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo na maarifa ya mtahiniwa katika mada ya zaka.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,484** sawa na asilimia **95.20** watahiniwa **226** sawa na asilimia **4.80** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 4b.


**Jadweli Nambari 4b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,864 | 41.57 | 2,175 | 48.51 | 445 | 9.92 | 2,620 | 58.43 |

Takwimu za jadweli nambari 4b zinaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **9.92** upo katika kiwango cha vizuri na kupelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **58.43.**

Aidha, watahiniwa **1,864** sawa na asilimia **41.57** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 8.1.

**Kielelezo (8.1) ( kibaya)**


8. a) Zakka kisheria ni miongoni mwa ibada njema

b) Wanaostahiki kupewa zakka kwa mujibu wa Qur-ani ni watu wa aina moja

c) Makundi manne (4) ya mwanzo ya watu wanaostahiki kupewa zakka ni


i. Kufanya ibada
ii. Kuto mkufuru mungu
iii. Kuwa na tabia njema
iv. Kuwa mtu mzuri

d) Ili zakka iweze kukubaliwa ni lazima itolewe mali iliyokuwa nzuri

Kielelezo nambari 8.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana hakuwa na maarifa ya kutosha juu ya alichoulizwa. Mtahiniwa huyu alitakiwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa mfano katika kipengele (a) alitakiwa kuandika maana ya zaka kisheria, lakini yeye aliandika maana hiyo kwa ufahamu wake.

Aidha watahiniwa **445** sawa na asilimia **9.92** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa pamoja na ufahamu mzuri juu ya mada ya zaka kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 8.2

**Kielelezo (8.2) ( kizuri)**



8. a) Zakka kisheria ni kipande cha mali kinachotolewa kwa ajili ya allah (s.w) ikipitiwa na mwaka na kupewa watu maalumu.

b) Wanaostahiki kupewa zakka kwa mujibu wa Qur-ani ni watu wa aina nane (8)

c) Makundi manne (4) ya mwanzo ya watu wanaostahiki kupewa zakka ni

i. Maskini.

ii. Mafakiri.

iii. wanaozitumikia zaka.

iv. muislamu aliesilimu.

d) Ili zakka iweze kukubaliwa ni lazima itolewe mali iliyokuwa halali

Kielelezo nambari 8.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na maarifa mazuri juu ya mada ya zaka, ambapo kwa mfano katika kipengele (c) ameweza kuorodhesha makundi manne ya mwanzo ya watu wanaostahiki kupewa zaka.

### 3.4.3 Swali la 9: Fiqhi

Swali hili lilimtaka mtahiniwa aeleze faida nne zinazopatikana katika ibada ya funga.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kueleza faida za funga.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,759** sawa na asilimia **79.81** watahiniwa **951** sawa na asilimia **20.19** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 4c.


**Jadweli Nambari 4c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,371 | 36.47 | 2,160 | 57.46 | 228 | 5.96 | 2,384 | 63.42 |

Takwimu za jadweli nambari 4c zinaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **5.96** upo katika kiwango cha vizuri, ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **63.42**.

Aidha watahiniwa **1,371** sawa na asilimia **36.47** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 9.1.

**Kielelezo (9.1) (kibaya)**



9. Eleza faida nne (4) zinazopatikana katika ibada ya funga.

- Kupunguza Sukari na Sumu kwa wingi mwilini
- ~~Kuzalis~~ Kuzalisha kwa celi nyekundu katika mwili.
- Ni jambo linalojaza mizani kwa kiwango kikubwa (amali njema).
- ~~At~~ Funga ni nguzo ya tano (5) katika uislamu ni lazima kwa kila

- Tunapata malipo makubwa kwa Allah (s.w) ~~ma~~ kupitia funga na malipo yake hayana ~~idadi~~ kiwango maalumu.
- Pia ni chanzo kwa kuzalishwa kwa celli nyekundu.
- Pia ~~ina~~ inasaidia kupunguza kwa kiwango cha Sukari na Sumu mwilini.
- Kuwa na afya.

Kielelezo nambari 9.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana hakuwa na maarifa ya kutosha juu ya alichoulizwa. Mtahiniwa huyu alitakiwa kueleza faida zinazopatikana katika funga, badala yake katika hoja zake mbili (hoja ya kwanza na hoja ya tatu) ameteja tu bila kueleza na hoja zilizobaki amekosa, hali ambayo imempelekea kufanya vibaya katika swali lake hili.

Aidha watahiniwa **228** sawa na asilimia **5.96** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa mazuri juu ya funga kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 9.2

**Kielelezo (9.2) ( kizuri)**

9. Eleza faida nne (4) zinazopatikana katika ibada ya funga.

a- Kujenga mahusiano mazuri baina ya mja na Mola wake: Kuweza kuwa karibu na Allah (s.w) na chochote kitakacho tokezea basi wewe upo tayari nalo.

b- Kumcha Mwenyezi Mungu: Kufanya Ibada mara kwa mara ukiwa upo ndani ya Mwezi wa kufunga na hata mwezi wa kula mchana, wewe ukawa unafanya Ibada, na unasoma Qur'ani kama ipasavyo

c- Kuwa na ~~shiha~~ siha nzuri katika mwili: Ukiwa umefunga basi katika mwili utaondokewa na maradhi na utakuwa na afya nzuri kabisa

d- Kusamehewa madhambi: Indapo utafunga unaweza kusamehewa madhambi ukifunga Sunna pia unaweza kulipwa thawabu na hata hiyo funga na ukaweza kukinai na kujizuia kula, kunywa na yale yote yanayofunguza na kuharibu Ibada yote ya Funga.

Kielelezo nambari 9.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na maarifa mazuri juu ya fungaa, ambapo ameweza kutoa hoja nne zinazohusiana na faida za funga pamoja na kuzielezea.

### 3.4.4 Swali la 10: Tohara

Swali hili lilimtaka mtahiniwa amfahamishe ndugu yake wa Kiislamu namna ya kujitoharisha na hadathi kubwa.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima matumizi kwa mtahiniwa juu ya namna ya kujitoharisha na hadathi kubwa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **1,028** sawa na asilimia **21.83** watahiniwa **3682** sawa na asilimia **78.17** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 4d.

**Jadweli Nambari 4d: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 720 | 70.04 | 269 | 26.17 | 39 | 3.79 | 308 | 29.96 |

Takwimu za jadweli nambari 4d zinaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **3.79** upo katika kiwango cha vizuri, ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **29.96.**

Aidha watahiniwa **720** sawa na asilimia **70.04** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na maarifa katika kufahamu namna ya kumfahamisha mtu juu ya kujitoharisha na hadathi kubwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 10.1.

**Kielelezo (10.1) (kibaya)**

10. Kulingana na mafundisho ya Mtume (S.A.W), mfahamishe ndugu yako wa kiislamu aliyepatwa na hadathi kubwa namna ya kujitoharisha kutokana na hadathi hiyo.

Maana ya mafundisho
Mafundisho ni maneno yenye vitendo au kauli ndani yake kwa ajili kuya fanyia kazi kwa vitendo katika mafundisho.
hadathi kubwa ni kama -> mbwa, nguruwe n.k.
hadathi kumbwa namna ya kujitoharisha kutokana na hadathi hii namna kujitoharisha ni kufanya tohara

ya hadathi mtu aliyeingia na hadathi anatakiwa
kufanya tohara ili kutoka na hadathi ile hadathi
na najisi na najisi husababishwa na wanyama au
mkojo wa mtoto mchanga: Mtu anapoingiya na hadathi
ni lazima kujitoharisha kwa sababu hadathi ni kusema
aidha ya maradhi au uchafu anapoingiya Mwislamu
lazima mtu afanye au afuate maelekezo wa
kufanya tohari inategeme na hadathi mtu aliyoingiya
aidha hadathi ndogo au hadathi ya kati na kati

au kubwa kwa muislamu muamini wa kweli
hawezi kukaa na hadathi hata mara moja au dakika
moja au sekonde moja na hadathi hii inasababishwa
na wanyama maalumu pale mtu anapowachezewa
au kuwashika wanyama hawa ndo hadathi
yenyewe wanyama tunatakiwa tunaenao mbali
na jamii au maadili ya kiislamu na tunusurike
na hadathi ya wanyama hawa wenye hadathi
na kufuata mashr mashrti ya muongozo nzima

wa dini wa kiislamu tunatakiwa tuwe na tabia
za mtume ya mtume S.A.W pamoja na maswahaba
zake

Kielelezo nambari 10.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana hakuwa na maarifa ya kutosha juu ya alichoulizwa. Mtahiniwa huyu alileta maelezo anayoyajua yeye ambayo ni kinyume na matakwa ya swali, hali ambayo imepelekea kufanya vibaya katika swali hili.

Aidha watahiniwa **39** sawa na asilimia **3.79** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa mazuri juu ya namna ya kutoharisha hadathi kubwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 10.2

**Kielelezo (10.2) ( kizuri)**

10. Kulingana na mafundisho ya Mtume (S.A.W), mfahamishe ndugu yako wa kiislamu aliyepatwa na hadathi kubwa namna ya kujitoharisha kutokana na hadathi hiyo.

Nitamfahamisha kwa kumwambia hadathi kubwa haiwezi kutoharika mpaka kwa kuoga na njia za kujitoharisha kama zifuatazo:-

(1) Ni kutia nia onia ni kama kwa kusema nina nuia kujitoharisha kutokana na hadathi kubwa

(2) Utatawadha vizuri kisha utatia udhu.

(3) kisha utaanza kujitia maji kuanzia kichwa ni kwenye utosi mpaka kwenye nyayo za miguu mara tatu (3).

(4) kisha utajitia maji upande wa kulia mara tatu (3) kuanzia kwenye kichwa mpaka kwenye nyayo.

(5) kisha utajitia maji upande wa kushoto mara tatu (3) kuanzia kwenye kichwa mpaka kwenye nyayo za miguu.

Kielelezo nambari 10.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na maarifa mazuri juu ya tohara, hali iliyopelekea kuweza kumfahamisha ndugu yake namna ya kujitoharisha na aina hiyo ya hadathi.

### 3.5 SEHEMU E: TAREKHE

Katika sehemu hii kulikuwa na maswali mawili (2) kutoka katika mada ya Tarekhe. Watahiniwa walitakiwa kuchagua swali moja tu (1) katika sehemu hii. Katika sehemu hii swali lake lilikuwa lina alama kumi (10).

### 3.5.1 Swali la 11: Tarekhe

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua matukio matatu yaliyomtokezea Mtume (S.A.W) wakati alipokuwa njiani kuelekea Madina.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa juu ya safari ya Mtume (S.A.W) kuelekea Madina.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **2,542** sawa na asilimia **53.97** watahiniwa **2,168** sawa na asilimia **46.03** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 5a.

**Jadweli Nambari 5a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,251 | 49.21 | 964 | 37.93 | 327 | 12.86 | 1,291 | 50.79 |

Takwimu za jadweli nambari 5a zinaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **12.86** upo katika kiwango cha vizuri, ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani wa asilimia **50.79.**

Aidha watahiniwa **1,251** sawa na asilimia **49.21** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 11.1.


**Kielelezo (11.1) (kibaya)**

11. Fafanua matukio matatu (3) yaliyomtokezea Mtume (S.A.W) alipokua njiani kuelekea Madina.

alipata shida nyingi katika safari yake aliyo kuwa anaelekea madina alipigwa mawe alitolewa maneno wasiyokuwa na maana alitukanwa matusi makubwa makubwa na kupata shida nyingi mpaka kufika madina walinsengenya na kum tolea maneno wata msaliti alipigwa mpaka akafika madina alipo fika

madini akapokewa kwa shwange na Vigelegele na ataimbiwa shairi ali furahi kwa akawa analiya furaha yake ilikuwa katika furaha ya maie na yake alifurahi tena alifurahi sana furaha yake haina kifani walimchukua na kumpokea mizigo yake na kuenda kuyeka ndani mas wahaba zake walimuuliza ukounapotota kujakutana na jambo lolote lile


alisema nime kutana na masha ka ambayo sija na wahi kuyaona ndo kuanza leo niyaone kili kutana na Makuraishi wamenipiga mpaka nika kosa nguvu za kuja huku nika muumba M Imungu anifikishe


madina ufalauma ualimini na Mlmungu
atanifikia ufalatma ualimini mpaka
nikafika hapa madina nanshukuru
Mlmungu ame ipotea dua yangu
ya kufika hapa madina maana
yake nimepijua mpaka nimeona sifiki
madina lakini mimemuomba na aka
isikia dua yangu
Tunatakia tuwiia na jambo tumshukur
u Mlmungu na atatutekelezea mambo
yetu yaende kwa ufalauma na amani?


Kielelezo nambari 11.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana amechanganya baina ya safari ya Mtume (S.A.W) ya kuelekea Madina na safari ya Mtume (S.A.W) ya kuelekea Taif, hali . ambayo anaonekana kwenda kinyume na matakwa ya swali, na kupelekea kufanya vibaya katika swali hili.

Aidha watahiniwa **327** sawa na asilimia **12.86** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa mazuri juu ya safari ya Mtume Muhammad (S. A. W) kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 11.2

**Kielelezo 11.2 (kielelezo kizuri)**


11. Fafanua matukio matatu (3) yaliyomtokezea Mtume (S.A.W) alipokua njiani kuelekea Madina.

MATUKIO MATATU YALIYO MTOKEZEA MTUME ALIPOKUA
NJIANI KUELEKEA MADINA.
Safari ya Mtu kutoka Makka kwenda Madina alifa
hiyo kwa Sababu Cha Mamuzi ya Makafiri Makafiri
Walitaka kumuua Mtume (S.A.W) na Usiku ule Makafiri wa-
likuwa washaizunguka Nyumba ya Mtume. Mtume
wakati wa Safari yake kulitokea Miujizi mingi
Nayo ni :-
i. Mtume alifatana na bubakar (ra) walifika njiani na


kamkata mbuzi alie zoeka na Mwenye mbuzi yu
po karibu na Mtume alikuwa ana kuu. Mtume
aliyo mkamata chuchu Mbuzi yule Mbuzi
apuapo maziwa yalijaa na kurea hali yake yakawa
na Maziwa Mara nyingi.
"2" Kuzama kwa farasi wa Suraka bin Malik. Suraka bin
Malik alikuwa kafiri alitumwa kwenda kumu
uwa Mtume Suraka na farasi wake walienda
Mpaka wakamkuta kila alipo sokea Suraka basi
alizama ndani ya torre apuapo Suraka aka
Silimu basi Suraka akaungana na Mtume kati
ka Safari yao.
"3" Al: Bui bui na Njiwa walitanda katika pango
alimo ingia Mtume. Mtume aliingia ndani
ya pando kujificha apuapo Mwenyezimungu alim
shusha buibui alietando katika mlango wa wa
pango na Njiwa aliye lalia Mayai yake ili
Makafiri watapo kuja waone haja ingia.
Kwa hivyo nasi tuna takiwa tulinganie dini
ya Allah na kufuata maamrisho yake

Kielelezo nambari 11.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na maarifa mazuri juu ya alichoulizwa, hali iliyopelekea kuweza kufafanua vizuri matukio ya njiani yaliyomkuta Mtume (S.A.W) alipokuwa akihama Makka kuelekea Madina.

### 3.5.2 Swali la 12: Kuhama Makka Mtume (S.A.W) kuelekea Madina

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza mafunzo yanayopatikana kupitia safari ya Mtume (S.A.W) ya kuhama Makka na kuelekea Madina.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ujuzi na maarifa ya mtahiniwa juu ya safari ya Mtume (S.A.W) kuelekea Madina.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **1,852** sawa na asilimia **39.32** watahiniwa **2,858** sawa na asilimia **60.68** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 5b.


**Jadweli Nambari 5b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 886 | 47.84 | 595 | 32.13 | 371 | 20.03 | 966 | 52.16 |

Takwimu za jadweli nambari 5b zinaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **20.03** upo katika kiwango cha vizuri, ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani wa asilimia **52.16.**

Aidha watahiniwa 886 sawa na asilimia **47.84** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 12.1.

**Kielelezo (12.1) (kibaya)**


12. Eleza mafunzo manne (4) tunayoyapata kupitia safari ya Mtume (S.A.W) ya kuhamia Makka na kuelekea Madina.

a) Kuwa na Subira
b) Kumu amini Allawa (S.W) popote Ulipo
c) Kujua kumba Allawa (S.W) yupo popote Ulipo
d) Kujua kwamba Allawa (S.W) hana mshirika

Kielelezo nambari 12.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana hakuwa na ufahamu juu ya alichoulizwa, hali iliyopelekea kuandika hoja zisizokubaliana na swali, hivyo kupelekea kufanya vibaya swali hili.

Aidha watahiniwa **371** sawa na asilimia **20.03** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa mazuri juu ya mafunzo yanayopatikana katika safari ya Mtume (S.A.W) ya kuhama kuelekea Madina kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 12.2

**Kielelezo 12.2 (kielelezo kizuri)**

12. Eleza mafunzo manne (4) tunayoyapata kupitia safari ya Mtume (S.A.W) ya kuhamia Makka na kuelekea Madina.

Kuhama ni kutoka sehemu moja kwenda Sehemu nyengine aidha kwa kuhama au kutembea ~~katika~~ mafunzo manne tunayoyapata kupitia safari ya Mtume (S.A.W) ya kuhamia Makka na kuelekea ~~Na~~ Madina ni :-

Kutunza siri :- Tunatakiwa tuwe tunatunza siri vovote iwavo ikibidi kufa.

Kutumia akili kushinda maadui :- Pindi makafiri wanapotaka kuvamia waislamu tunatakiwa tutumie akili.

Kuwa muaminifu kwa kurejesha amana : Tunapopewa amana ya watu tunatakiwa kurejesha ikiwa vilevile isipungue hata kidugu.

Huruma na upole ~~na~~ na heshima ya mtume S.A.W : Kama Kiongozi alikuwa na heshima na sisi tunatakiwa ~~kurejesha~~ kuwa kama alivyokuwa yeye Kiongozi wetu mtume (S.A.W)

Kutokana na maelezo yaliyopo hapo juu yanaonyesha mafunzo kupitia Safari ya mtume (S.A.W) kuhama makka kwenda madina.

Kielelezo nambari 12.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa na maarifa mazuri juu ya alichoulizwa, hali iliyopelekea kuweza kueleza mafunzo yanayopatikana kupitia safari ya Mtume (S.A.W) kuhama Makka kuelekea Madina.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa jumla wa ufaulu unaonesha kuwa maswali manne yalijibiwa vizuri na maswali nane yalijibiwa wastani na hakuna swali lilijibiwa chini ya wastani.

Uchambuzi wa jumla unaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa walishindwa kupata ufaulu mzuri kutokana na ufahamu mdogo kwa mada mbalimbali zilizoulizwa pamoja na uwezo mdogo wa kujibu maswali hasa ya kuelezea.

Mwisho, taarifa hii ya kufaulu itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu wa somo hili la dini ya Kiislamu kwa kiwango kizuri zaidi Inshaallah.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha somo la dini ya Kiislamu katika ufaulu wake, yafuatayo ndio yanayo pendekezwa:

i) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ifanye juhudi kwa kuwatafuta wafadhili wa nje na ndani ya nchi, watakaowezesha kutungwa kwa vitabu vya somo la dini ya Kiislamu kama ilivyo kwa masomo mengine.

ii) Walimu wa somo la dini ya Kiislamu wajitahidi kumaliza muhtasari katika somo la dini ya Kiislamu.

iii) Kupatiwa walimu semina mbalimbali kuhusiana na kujifunza na ufundishaji kwa somo la dini ya Kiislamu katika ngazi ya msingi.

iv) Walimu wawe na tabia ya kujitolea katika kununua vitabu mbalimbali vya kusomeshea somo la dini ya Kiislamu.

v) Walimu wajitahidi kuwapa wanafunzi wao mitihani yenye viwango wakati wanapowatahini.

vi) Walimu wawape wanafunzi wao mazoezi kwa wingi ya kazi za kueleza na kuwapa maelekezo juu ya maswali ya aina hiyo.

vii) Walimu washajiishe wanafunzi kupenda somo la Dini.

viii) Walimu wajitahidi kuwajengea uwezo na ujuzi wa kivitendo wanafunzi wao kwa mada zinazohitaji vitendo.

## VIAMBATANISHO

### KIAMBATANISHO NAMBARI 1

### UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA MWAKA 2023

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Tawhild | 4 | **97.40** | **VIZURI** |
| 2 | Qur - ani | 1 | **90.74** | **VIZURI** |
| 3 | Fiqhi na Maadili | 7 | **87.77** | **VIZURI** |
| 4 | Fiqhi na Maadili | 9 | **63.42** | **WASTANI** |
| 5 | Hadithi | 6 | **59.42** | **WASTANI** |
| 6 | Fiqhi na Maadili | 8 | **58.43** | **WASTANI** |
| 7 | Tawhild | 3 | **55.08** | **WASTANI** |
| 8 | Tarekh | 12 | **52.16** | **WASTANI** |
| 9 | Tarekh | 11 | **50.79** | **WASTANI** |
| 10 | Qur - ani | 2 | **49.36** | **WASTANI** |
| 11 | Hadithi | 5 | **44.84** | **WASTANI** |
| 12 | Fiqhi na Maadili | 10 | **29.96** | **WASTANI** |

### KIAMBATANISHO NAMBARI 2

### UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA MWAKA 2022

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Tawhild | 4 | **96.28** | **VIZURI** |
| 2 | Qur - ani | 1 | **85.28** | **VIZURI** |
| 3 | Fiqhi na Maadili | 7 | **80.35** | **WASTANI** |
| 4 | Fiqhi na Maadili | 8 | **81.61** | **WASTANI** |
| 5 | Tawhild | 3 | **58.11** | **WASTANI** |
| 6 | Fiqhi na Maadili | 9 | **40.91** | **WASTANI** |
| 7 | Fiqhi na Maadili | 10 | **37.36** | **WASTANI** |
| 8 | Tarekh | 11 | **34.00** | **WASTANI** |
| 9 | Hadithi | 5 | **33.13** | **WASTANI** |
| 10 | Hadithi | 6 | **28.47** | **WASTANI** |
| 11 | Tarekh | 12 | **25.00** | **WASTANI** |
| 12 | Qur - ani | 2 | **22.93** | **WASTANI** |